



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO**

MAMLAKA YA AFYA YA MIMEA NA VIUATILIFU (TPHPA)

TANGAZO LA ZABUNI YA KUMPATA FUNDI UJENZI

TAREHE: 16/05/2022

1. Mamlaka ya **TPHPA** [Zamani ikijulikana kama TPRI] imetenga fedha katika Bajeti yake ya Mwaka wa Fedha 2021/2022 kwa ajili ya **Ukarabati wa jengo la Maktaba.**
2. Mkurugenzi Mkuu wa **TPHPA** anawaalika mafundi wenye sifa kuleta gharama zao za kazi za ufundi kama tangazo linavyojieleza
3. Utaratibu utakaotumika katika mradi huu ni **FORCE ACCOUNT** ambapo vifaa vyote vya ujenzi vitanunuliwa na **TPHPA**
4. Fundi atapatikana kwa njia ya ushindani wa gharama ya kazi kwa kuzingatia sifa zilizoainishwa hapa chini:

SIFA ZA FUNDI

- I. Awe mwenye uwezo wa kusoma na kutafsiri ramani na michoro.
- II. Mwombaji aoneshe uzoefu wake sehemu alizowahi kufanya kujenga (ambatanisha mkataba wa kazi uliyowahi kufanya)
- III. Mwombaji aoneshe muda atakao tumia kukamilisha kazi.
- IV. Mwombaji aoneshe bei yake kwa kuonyesha mchanganuo wa bei ya kila hatua za kazi.
- V. Mwombaji aambatanishe barua ya utambulisho toka ofisi ya Mtendaji wa kijiji/kitongoji/Mtaa anakoishi/anakotokea.
- VI. Mwombaji anatakiwa awe na kitambulisho kimoja kati ya hivi (kitambulisho cha Taifa, (NIDA) kitambulisho cha Mpiga Kura, Leseni ya Udereva au Hati ya Kusafiria)

- VII. Mwombaji anatakiwa kuwa na wadhamini wawili (wadhamini wanatakiwa kuwa na vitambulisho vya Taifa, Kitambulisho cha Mpiga Kura, Leseni ya udereva au Hati ya Kusafiria)
- VIII. "Schedule of Labour's zitapatikana kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni TPHPA
- IX. Gharama ya zabuni hii ni shilingi 10,000/= ambazo hazitarudishwa iwapo fundi atakosa kazi.
5. Fundi ni lazima afike kuliona Jengo la Makataba na kutathmini ukubwa wa kazi kabla ya kujaza gharama za mafundi.
6. Barua /nukuu zote za gharama zikiwa zimejazwa vizuri na kufungwa katika bahasha, juu ya bahasha zikiwa zimeandikwa, **Ukarabati wa Jengo la Maktaba** na ziwasilishwe katika ofisi ya **Katibu wa Bodi ya Zabuni TPHPA – Makao Makuu S.L.P 3024, Arusha- Ngaramtoni.**
7. Mwisho wa kupokea zabuni (maombi) ni tarehe 25/05/2022 siku ya Jumatano saa nne kamili asubuhi katika ukumbi wa mikutano wa TPHPA. Maombi yatafunguliwa kwa uwazi mbele ya mafundi watakaopenda kuhudhuria ufunguzi mara baada ya kupokelewa.
8. Nukuu za bei zitakazo cheleweshwa, ambazo hazijapokelewa na ambazo hazikufunguliwa wakati wa ufunguzi hazitapokelewa wala hazitashughulikiwa.
9. Siku za kutoa ufafanuzi [Clarification] kuhusu ukarabati tajwa hapo juu utafanyika kuanzia tarehe 18 – 20 Mei, 2022 katika ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni TPHPA, kuanzia saa nne kamili (4.00) asubuhi hadi saa tisa (9.00) kamili alasiri.

IMETOLEWA NA:

KNY: KAIMU MKURUGENZI MKUU
MAMLAKA YA AFYA YA MIMEA NA VIUATILIFU (TPHPA)



Jiandae Kuhesabiwa Siku ya Jumanne tarehe 23 Agosti, 2022